Nambari ya Mtahiniwa ____________________

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**107** **DINI YA KIISLAMU**

**MUDA: SAA 2:30** **JUMANNE 15 OKTOBA, 2024 MCHANA**

---

## MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu TANO (5) A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, B na C, maswali MATATU (3) kutoka sehemu D, swali la SABA (7) ni lazima. Jibu swali MOJA (1) kutoka sehemu E.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu ya mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |
| JUMLA | | |
| SAINI YA MHAKIKI | | |

0072473

Mtihani huu una kurasa 14 zenye maandishi

**Nambari ya Mtahiniwa ____________________**

## SEHEMU A: (Alama 20)

## QUR-ANI NA TAFSIRI

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. Chagua jawabu sahihi na uandike herufi yake katika jadweli lililopo chini.

i. Katika neno " إِنَّ رَبَّهُمْ بِهِمْ " inapatikana hukumu ya

A: idh-haar haqiqiyu  B: idh-haar shafawiyu

C: ikhfau haqiqiyu  D: ikh-faau shafawiyu

ii. "Na kitu gani kitakachokujuilisha hicho kiyama?" Tafsiri hii inapatika katika sura gani?

A: Adiyaat  B: Bayyinah

C: Qariah  D: Qadri

iii. Bainisha hukumu ya mimu sakina inayopatikana katika aya hii

"وَخَلَقْنَاكُمْ أَزْوَاجًا"

A: id-gham mutaqaribain  B: id-gham mutamaathilayni

C: idh-har haqiqiyu  D: idh-har shafawiyyu

iv. Suratul Tyn ina aya ngapi?

A: 6  B: 7

C: 8  D: 9

v. Tunajifunza nini kupitia aya (1 - 5) ya Suratul Alaq?

A: kusoma kwa ajili ya Allah (S.W)

B: kusoma kwa ajili ya maendeleo

C: kusoma kwa ajili ya Masahaba

D: kusoma kwa ajili ya Mtume (S.A.W)

vi. Hukumu za mimu sakina zimegawika katika vigawanyo vingapi?

A: vitatu  B: vinne

C: vitano  D: sita

vii. Ni ipi tafsiri sahihi ya aya ya tano ya Suratul-Zilzalah?

A: na ardhi itakapotowa mizigo yake

B: na binaadamu atakaposema leo ardhi ina nini?

C: kwa kuwa Mola wako ameiamrisha

D: siku hiyo ardhi itahadithia habari zake

viii. Qur-ani ina jumla ya sura ngapi?

A: 113 B: 114

C: 115 D: 116

ix. Inapendeza kwa mwenye kusoma Qur-ani awe na

A: ukarimu B: upole

C: huruma D: udhu

x. "Hakika ya mwanadamu yuko katika hasara". Tafsiri ya aya hii inapatikana katika sura gani?

A: Asri B: Balad

C: Kauthar D: Takaathur

**JAWABU**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. a) Soma aya zifuatazo kisha andika tafsiri ya kila aya.

١. إِلَّا الَّذِيْنَ آمَنُوا وَعَمِلُوْا الصّٰلِحٰتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

٢ . ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُوْنَ.

___________________________________________

___________________________________________

٣ . فِيْهَا كُتُبٌ قَيِّمَةٌ.

___________________________________________

___________________________________________

٤ . إِنَّ رَبَّهُمْ بِهِمْ يَومَئِذٍ لَّخَبِيْرٌ.

___________________________________________

___________________________________________

٥ . بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَى لَهَا.

___________________________________________

___________________________________________

b) Panga tafsiri ya aya zifuatazo kwa usahihi wake kisha andika herufi katika jadweli lililopo chini.

A. Naye anajua haya.

B. Na yatakapodhihirishwa yaliyomo vifuani.

C. Je! Hajui watakapofufuliwa waliomo makaburini?

D. Bila shaka mwanadamu atamkanusha Mola wake.

E. Na ana mapenzi makubwa kabisa ya kupenda mali.

**JAWABU**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

Nambari ya Mtahiniwa ____________________

**SEHEMU B: (Alama 20)**

**TAWHIDI**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

3. Chagua jawabu sahihi ya tafsiri ya majina ya Mwenyezi Mungu kutoka **ORODHA A** kwa kulinganisha na majina ya Mwenyezi Mungu kutoka **ORODHA B** kisha andika herufi yake kwenye jadweli lililopo chini.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Mwenye uwezo wa kusubiri | A- الْبَرُّ |
| ii. Mwenye uwezo wa kuongoza | B- الضَّارّ |
| iii. Mwenye uwezo wa kubakia | C - الرَّؤُوْفُ |
| iv. Ni mmoja | D- الظَّاهِرُ |
| v. Aliyedhahiri | E - الْوَاحِدُ |
| vi. Mwema kwa waja wake | F - الْآخِرُ |
| vii. Ni wa mwisho | G- الْبَاقِي |
| viii. Mwenye huruma | H - الْهَادِي |
| ix. Mwenye nuru | I- الْمُغْنِيْ |
| x. Mwenye kudhuru | J- الصَّبُوْرُ |
| | K- النُّوْرُ |
| | L - الْمُهَيْمِنُ |

**JAWABU**

| **ORODHA A** | i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **ORODHA B** | | | | | | | | | | |

4. Andika herufi “**K**” kwa ibara iliyokuwa sahihi na herufi “**S**” kwa ibara isiyokuwa sahihi katika jadweli lililopo chini.

   i. Mwenye kuyafanyia kazi majina ya Allah (S.W) ataingia peponi.
   ii. Mwenye kuabudia jua atakuwa ametoka katika uislamu.
   iii. Kuna aina nne (4) za unafiki kwa mujibu wa hadithi ya Mtume (S.A.W).
   iv. Lukman (A.S) ni mtume wa sita katika orodha ya mitume.
   v. Kisheria imani ni kuamini moyoni juu ya kila kitu.
   vi. Al-qadir ni jina la Allah (S.W) lenye maana ya “ mwenye uwezo”.
   vii. Imani ya mwanadamu inazidi na kupungua kulingana na matendo.
   viii. Shirki ya aina yoyote humtoa mja katika uislamu.
   ix. Mnafiki ni mtu ambae anapatikana katika waislamu.
   x. Abdallah bin Ubayya bin Salul alikuwa kiongozi wa wanafiki.

**JAWABU**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

## SEHEMU C: (Alama 20)

## HADITHI

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

5. Kamilisha hadithi ifuatayo kwa kuchagua jawabu sahihi katika mabano.

( عَنْهُ، حَلاَوَةَ، ثَلاَثُ، مَالِكِ، مِمَّا، مِنْهُ، يَعُوْدَ، فِيْهِ، الله، يُحِبَّ، أَرْبَعُ، عَنْهُمَا)

عَنْ أَنَسِ بْنِ __________ رَضِيَ اللهُ __________ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ

وَسَلَّمَ قَالَ: __________ مَنْ كُنَّ __________ وَجَدَ بِهِنَّ

__________ الْإِيْمَانِ أَنْ يَكُوْنَ اللهَ وَرَسُوْلَهُ أَحَبَّ إِلَيْهِ __________

سِوَاهُمَا وَأَنْ ____________ الْمَرْأَ لَا يُحِبُّهُ إِلَّا ____________

وَأَنْ يَكْرَهَ أَنْ ____________ فِيْ الْكُفْرِ بَعْدَ أَنْ أَنْقَذَهُ اللهُ ____________

كَمَا يَكْرَهُ أَنْ يُقْذَفَ فِيْ النَّارِ.

6. a) Andika tafsiri ya maneno yafuatayo:

- حَلاَوَةَ ____________________________________________
- الْحَسَنَةَ ____________________________________________
- مَجَالِسُنَا ____________________________________________
- ضَيْفَهُ ____________________________________________
- مُسْكِرٍ ____________________________________________

b) Toa mafunzo mawili (2) ambayo waislamu wa leo wanajifunza kutokana na hadithi ya ubaya wa wizi.

i. ____________________________________________
____________________________________________

ii. ____________________________________________
____________________________________________

**SEHEMU D: (Alama 30)**

**FIQHI NA MAADILI**

**Jibu maswali MATATU (3) katika sehemu hii, likiwemo swali la SABA (7).**

7. Kamilisha nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika jibu lililosahihi.

i. Miongoni mwa ubaya wa utandawazi ni ______________________
____________________________________________ na
____________________________________________

ii. Mama ana wajibu wa ______________________________ mwanawe kwani _______________________ ya mama ni lishe bora kwa mtoto.

iii. Maadili ya kiislamu ni utaratibu na mfumo wa kumjenga _____________________ kuwa ni mja wa __________________ kama alivyoagizwa.

iv. Miongoni mwa njia za kuepukana na uasharati ni kumuogopa ________________________ na kuidhibiti nafsi kwa yale yote ambayo Allah (S.W) na Mtume wake __________________________

v. Mke wa kiislamu anakuwa makosani anapotoka nje ya __________________ bila ya ruhusa ya ________________________

8. Sala ya maiti ni faradhi kifaya. Eleza namna utakavyoitekeleza sala hiyo.

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

9. Babu Rahim anajitayarisha kwenda Makka kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Hijja. Mfahamishe kwa umakini masharti manne (4) ya ibada hiyo.

10. Muislamu hawezi kufanya ibada yoyote bila ya kuwa tohara. Fafanua hatua utakazozichukua katika kumfunza mtu asiyejua kujitoharisha na hadathi kubwa ya hedhi ili aweze kuendelea na ibada zake nyengine.

**Nambari ya Mtahiniwa** ____________________

## SEHEMU E: (Alama 10)

## TAREKHE

**Jibu swali MOJA (1) katika sehemu hii.**

11. Kwa kutumia hoja tatu (3) eleza jinsi Mtume (S.A.W) alivyofanikisha kujenga udugu baina ya Ansari na Muhajirina.

12. Mtume (S.A.W) alipofika Madina alikabiliwa na mambo muhimu ya kujenga jamii ya Kiislamu kwa wakati huo. Eleza mambo manne (4) ambayo aliyafanya katika kujenga jamii ya Kiislamu.

----------------------------------------------------